

**TAARIFA FUPI YA YALIYOONGELEWA KWENYE UAMUZI WA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA (MASJALA KUU)**

SHAURI LA KIKATIBA NA. 37 LA 2015

KATI YA

AMY P KIBATALAMWOMBAJI

NA

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALIMJIBU MAOMBI NA.1
MKURUGENZI WA TUME YA TAIFA YA**

UCHAGUZI TANZANIA MJIBU MAOMBI NA. 2

Kwa sababu na misingi inayoongoza tafsiri rasmi za sheria kama ambavyo tumeainisha kwenye uamuzi wetu rasmi (kwa kiingereza, hatuna shaka ya kwamba kifungu cha 104 (1) Sheria ya Uchaguzi [Sura ya 343 – 2002] ni kifungu cha kuweka marufuku kwa mtu yeyote kufanya mambo yaliyoainishwa, katika maeneo mahsusi na kwa wakati maalum, na kulifanya kuwa kosa la jinai kwa yeyote yule atakayefanya hayo yaliyopigwa marufuku, na kwa kosa hilo la jinai, mhusika anaweza kwa mujibu wa kifungu kidogo 104 (2) kushitakiwa Mahakamani kwa kosa hilo la jinai na iwapo ataonekana kuwa na hatia, kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Kifungu hicho cha sheria hakitoi maelekezo juu ya kufanyika kwa jambo lolote. Ni kifungu jinai – hivyo kinatakiwa kutafsiriwa moja kwa moja pasipo kuingiza maana ambayo haikukusudiwa na Bunge.

Kwa kuzingatia vigezo hivyo kifungu hicho kinatakiwa kusomeka na kuleta maana ifuatayo:

- “a) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuitisha au kufanya mkutano wa aina yoyote siku ya uchaguzi mahsusi kuwa ya kufanyika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, au katika eneo la jimbo la uchaguzi kunakofanyika uchaguzi – wa Mbunge [Tafisiri hiyo inatumika pia sawia kwa Kifungu cha 103 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292].*
- b) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvaa au kuonesha, kadi picha yoyote, upendeleo au nembo nyingine inayoonyesha kuunga mkono mgombea fulani katika uchaguzi, ama ndani ya jengo ambamo zoezi la kupiga kura linafanyika au kuendelea,*
- c) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvaa au kuonyesha kadi au picha yoyote, upendeleo au nembo nyingine inayoonyesha kuunga mkono mgombea fulani katika uchaguzi, popote pale ndani ya wigo wa mita 200 kutoka kituo ambapo zoezi la uchaguzi linafanyika, au ambapo zoezi la kuhesabu kura linapofanyika.”*

Kwa mujibu wa kufungu 104 (2), yeyote atakeyefanya lolote kati ya hayo yaliyokatazwa na 104 (1) atakuwa ametenda kosa la jinai.

2. Kwa kuwa makatazo yanayodaiwa kukiuka haki za binadamu za mdai au (mpiga kura)/mtu mwingine yeyote anayetaka kufuatilia zoezi zima la upigaji na kuhesabiwa kwa kura, ni makatazo kwa mujibu wa sheria mahsusi ya Bunge, ni makatazo halali kwa mujibu wa Katiba.
3. Kutokana na uamuzi huo – mdai amefanikiwa katika madai yake kwa kiwango cha kupata tafsiri sahihi ya kifungu cha sheria kama alivyoomba. Kwa upande wa pili, hakufanikiwa katika ombi la pili la dai la kukiukwa kwa haki yake ya kusimama au kuwepo umbali wa mita 200 kutoka kwenye kituo cha kupiga kura.
4. Kwa kuzingatia maslahi mapana ya umma yaliyoambatana na kuwepo ya haja ya kutafisiriwa kwa Kifungu hicho – 104 (1) cha Sheria ya Uchaguzi – Mahakama haioni kama kuna haja ya kuubebesha upande wowote gharama za shauri hili.

E.B. Luvanda

NAIBU MSAJILI

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

